***Ujumbe muhimu:*** kuanzia Februari tarehe 1, 2021, Kaunti ya King itaendesha vituo vya kutoa chanjo ya COVID-19 katika eneo la Auburn na Kent ili kuhudumia watu wa kusini mwa Kaunti ya King ambao ni 1) watu wenye umri wa miaka sabini na tano na zaidi, au 2) watu wenye umri wa miaka hamsini na zaidi ambao hawawezi kuishi kwa kujitegemea ,au ambao wanaishi na kuhudumia/kushughulikia watu wa familia zao, au 3) mtoa huduma/mfanyakazi wa huduma za nyumbani.kila kituo kitatoa hadi chanjo mia tano za bure kila siku. Vikundi vya ziada vitakua na uwezo wa kupanga kupokea chanjo katika vituo hivi kwa kujiandikisha wakati vifaa vya chanjo vitakapoongezeka.

**Ni nani anaweza kupokea chanjo katika vituo vya kutolea chanjo vya Auburn na Kent?**

Vituo hivi vinahudumia watu wanaoishi katika maeneo ya kusini mwa Kaunti ya King na ambao ni:

- Watu wenye umri wa miaka sabini na tano na zaidi
- Watu wenye umri wa miaka hamsini na zaidi na ambao:
    - **Hawawezi kuishi kwa kujitegemea** na wanapokea huduma kutoka kwa mtoa huduma, jamaa,mtoa huduma wa huduma ya nyumbani au mtu anayefanya kazi nje ya nyumba.
    - **Wanaishi na kuhudumia/kushughulikia wanafamilia/watu wa familia**. Mifano ni kama kuwashugulikia wajukuu, wapwa. Hii haihusishi wazazi wanaoishi na watoto wao.
- Mtoa huduma au mfanyakazi wa huduma za nyumbani anayemhudumia mtu mwenye umri wa miaka hamsini au zaidi na ambao hawawezi kuishi kwa kujitegemea. Mtoa huduma au mfanyakazi wa huduma za nyumbani anastahiki kuhudumu kama mfanyakazi katika mazingira ya huduma ya afya na wanaweza kuwa na umri wa chini ya miaka hamsini.

**Je kujiandikisha/kujisajili kunahitajika?**

- Ndio. Ikiwa utakidhi vigezo vya ustahiki na ungependa kupata chanjo, unaweza kujisajili/kujiandikisha kwa tovuti ya kingcounty.gov/covid/registration. [**Tovuti hii inapatikana kwa lugha ya kiingereza tu**]
- Je unahitaji usaidizi kujiandikisha kupitia kwa njia ya simu au na wakalimani? Piga simu kwa **nambari ya simu ya dharura ya usaidizi wa COVID-19 ya Jimbo la Washington** 1-800-525-0127 na ubonyeze alama ya # ili upate usaidizi wa kujiandikisha kupitia kwa njia ya simu. Kwa tafsiri ya lugha sema lugha unayoipenda wakati unawasiliana.
- Kwa sasa, usambazaji wa chanjo na kujiandikisha/kujisajili kunapatikana kwa uchache mno. Unaweza kucheleweshwa kwa sababu ya idadi kubwa ya watu wanaouliza/kutaka kujua zaidi. Hii itarahisishwa kama watoa huduma watapokea dozi zaidi na vituo vingi zaidi vya kutoa chanjo vitafunguliwa.

**Kwa nini kliniki hizi ni za watu wazee pekee na walezi wao katika eneo la kusini mwa Kaunti ya King?**

- Watu wenye umri wa zaidi ya miaka sabini na tano katika Kaunti ya King wamekuwa na viwango vya juu zaidi vya kulazwa hospitalini na kufa kutokana na ugonjwa wa COVID-19 kuliko kundi lolote lile.Asilimia sitini na tano ya vifo kutokana na COVID-19 katika Kaunti ya King vimekuwa vya watu wenye umri wa miaka sabini na tano na zaidi, ikilinganishwa na asilimia kumi na nane (18%) ya vifo kati ya watu wenye umri wa miaka sitini na tano hadi sabini na nne (65-74).
- Watu wenye umri wa zaidi ya miaka sabini na tano wana changamoto nyingi zaidi za kupata chanjo, kama vile usafiri na kutumia mitandao.
- Kusini mwa kaunti ya King kumeshuhudia idadi kubwa zaidi ya kesi hizi. kuwakinga wazee katika eneo hilo ndio tunakupa kipaumbele, hasa wale wanaoishi kati nyumba ambazo zina watu wa rika mbalimbali.
- Wakati vifaa vya chanjo havipatikani kwa urahisi, Kaunti ya King inahakikisha kuna usawa katika kupata chanjo hasa kwa wale wazee ambao wamo katika hatari kubwa zaidi na wanaishi katika

maeneo ambayo yana kesi nyingi zaidi za COVID-19.vikundi vya ziada vitaweza kupata chanjo katika vituo hivi wakati chanjo zaidi itapatikana.

Ni **nini ninahitaji kuja nacho kwa Miadi?**
Tafadhali kuja na kitambulisho cha picha yenye tarehe yako ya kuzaliwa. Hutarudishwa ikiwa huna kitambulisho. Ikiwa una bima ya afya,leta/beba nakala yako ya kadi ya bima. Tafadhali vaa shati ya mikono mifupi au nguo yenye mikono inayoweza kukunjika/kukunjwa.

**Nitalipishwa chochote?**
Unaweza kupata chanjo *bila malipo yoyote*, ikiwa una bima au huna bima. Ikiwa wewe una bima, utaulizwa kutoa/kupeana maelezo kuhusu bima yako.

**Sijasajiliwa/sijaandikishwa. Ni naweza kupata chanjo?**
Ndio. Hutaulizwa utoe idhibati yoyote ya uraia au unakoishi.

**Je vituo vya kupokea chanjo vinawapa watu chanjo wakiwa garini au wakiwa wanatembea kwenda huko?**
Kituo cha Auburn ni kituo kinachotoa chanjo kwa watu wakiwa ndani ya gari. Kituo cha Kent ni kituo kinachotoa chanjo kwa wamarekani walemavu bila kujiandikisha/kujisajili ADA . katika kliniki ya Kent, utahitajika kutoka katika sehemu ya kuegesha magari hadi ndani ya kituo cha ShoWare.

**Je utafsiri utapatikana katika vituo vya kutolea chanjo?**
Ndio, kutakuwa na tasiri ya lugha kwa baadhi ya luha zinazopatikana.

**Vituo vya kutoa chanjo havipatikani kwa urahisi kwangu. Ninaweza kupata chanjo kwa njia gani nyingine?**

- Piga simu kwa afisi ya daktari wako au mhudumu wa afya ili ujue ikiwa wanawaandikisha/wanawasajili watu ili wapate chanjo.
- Ikiwa huna mhudumu wa afya au mhudumu wako wa afya hana chanjo, tumia zana ya Jimbo la Washington ya kutafuta mtandaoni ili upate orodha ya maeneo ya kutoa chanjo: www.FindYourPhaseWA.org
- Ikiwa huwezi kutumia zana hiyo ya kutafuta mtandaoni na hakuna yeyote anayeweza kukusaidia kuitumia, unaweza kupata usaidizi kupitia kwa simu. Piga simu kwa nambari ya simu ya dharura ya usaidizi wa COVID-19 ya Jimbo la Washington**:** 1-800-525-0127, kisha bonyeza alama ya #. Inapatikana Jumatatu-Ijumaa: saa kumi na mbili asubuhi – saa nne usiku. Jumamosi, Jumapili, na likizo za serikali: saa mbili asubuhi – saa kumi na mbili jioni.kwa tafsiri ya lugha sema lugha unayoipenda wakati unapowasiliana.

**Je chanjo za COVID-19 ni salama?**
Chanjo za COVID-19 ni mpya na inaeleweka ikiwa utakuwa na maswali. Chanjo za COVID-19 zilitengenezwa kwa haraka, lakini watafiti wamekuwa wakisomea teknolojia iliyotumika kutengenezea chanjo kwa miaka mingi sana. Kwa kuongezea, maelfu ya watu kutoka rika tofauti,jamii ,makabila , na wenye hali mbalimbali za kimatibabu walishiriki katika utafiti wa kuhakikisha kwamba chanjo ya COVID-19 ni salama kwa kila mtu. Kama ilivyo kwa chanjo zote, chanjo ya COVID-19 itaendelea kufuatiliwa kwa sababu ya usalama zikiwa zinatumika.

**Ninaweza kupata wapi maelezo zaidi?**
Ikiwa una maswali kuhusu chanjo ya COVID-19 au ungependa maelezo zaidi kuhusu namna ya kupata chanjo katika Kaunti ya King, tafadhali tembelea tovuti ya www.kingcounty.gov/covid/vaccine [Tovuti hii inapatikana kwa kiingereza]